USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA USIMAMIZI WA MALIASILI

MWONGOZO WA MAFUNZO

YALIYOMO

SHUKRANI **4**
DIBAJI **5**
UTANGULIZI **6**

SEHEMU YA KWANZA **7**
USIMAMIZI **7**
SURA YA KWANZA **7**
USIMAMIZI WA MALIASILI ZA MISITU NA WANYAMAPORI **7**
1.0. Utangulizi 7
1.1. Maliasili ni nini? 7
1.2. Usimamizi wa Maliasili 7
1.3. Malengo ya Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori 7
1.4. Faida za Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori: 8

SURA YA PILI **9**
NJIA ZA USIMAMIZI WA MISITU NA WANYAMAPORI **9**
2.0 Utangulizi 9
2.1 Njia za Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori 9
2.1.1 Usimamizi wa Kuamrisha 9
2.1.2 Usimamizi wa Maliasili wa Kijamii 9
2.1.3 Usimamizi wa Mabadiliko-Mnyumbuko (Adaptive management) 9
2.1.4 Usimamizi wa Maliasili Jumuishi/Mkamilifu; 10

SURA YA TATU **11**
TAASISI ZA USIMAMIZI WA MISITU NA WANYAMAPORI **11**
3.0 Utangulizi 11
3.1 Taasisi za Usimamizi wa Misitu Tanzania 11
Serikali Kuu 11
Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania 11
Serikali za Mitaa 12
Serikali za Vijiji. 12
3.2.1 Taasisi za Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania 12

SEHEMU YA PILI **14**
SURA YA KWANZA **14**
SERA, SHERIA NA KANUNI ZINAZOHUSIANA NA MALIASILI **14**
1.0 Utangulizi 14
1.1 Sera ni nini? 14
1.1. Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998 14
1.2. Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 15
1.3. Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 15

SURA YA PILI **16**
SHERIA ZINAZOHUSU USIMAMIZI WA MISITU NA WANYAMAPORI **16**
2.0 Sheria ni nini? 16
2.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Namba 2 ya Mwaka 1977 16
2.2 Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999 16
2.3 Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999 17
2.4 Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Namba 7 ya Mwaka 1982 .. 17
2.5 Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Namba 8 ya Mwaka 1982..... 18
2.6 Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 20 ya Mwaka 2004 18
2.7 Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002 19
2.8 Sheria zinasosimamia Wanyamapori Tanzania 19
2.8.1 Sheria ya Hifadhi za Taifa ya Mwaka 1959 19
2.8.2 Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009 19

SURA YA TATU **21**
KANUNI, MIONGOZO NA ADHABU **21**
3.0 Kanuni ni nini? 21
3.1 Miongozo 21
3.1.1 Mwongozo wa Uvunaji Endelevu wa Misitu wa Mwaka 2007 21
3.1.2 Kanuni za Uanzishwaji wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Mwaka 2012. 21
3.2 Makosa na adhabu katika sheria za Misitu 22
3.3 Makosa na adhabu katika sheria za wanyamapori 25

SEHEMU YA TATU **27**
USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA USIMAMIZI WA MISITU NA WANYAMAPORI .. **27**
SURA YA KWANZA **27**
1.0. Utangulizi 27
1.1 Misingi ya Utawala bora katika Usimamiziwa Misitu na Wanyamapori 27
1.2 Ushiriki ni nini? 28
1.3 Umuhimu wa Kushiriki katika Usimamizi wa misitu na wanyamapori 28
1.2.1 Ushiriki wa Wananchi Katika Usimamizi Wa Misitu 28
1.3.2 Dhana ya Ugatuaji wa Madaraka katika Utekelezaji wa Miradi Shirikishi 29
1.3.3 Haki na Wajibu wa Wadau Mbalimbali 29
1.4 Ushiriki wa Wananchi Katika Usimamizi wa Wanyamapori. 30

SURA YA PILI **32**
CHANGAMOTO KATIKA USIMAMIZI WA MISITU NA WANYAMAPORI **32**
2.0. Utangulizi 32
2.1. Changamoto katika Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori 32
2.1.1. Kukinzana kwa Sheria 32
2.1.2. Mgongano wa Mamlaka za Kiutendaji katika Taasisi za Serikali 33
2.1.3. Ushiriki mdogo wa Wananchi katika Kutoa Mawazo yao na Kusimamia Kikamilifu Utunzaji na Uhifadhi wa Misitu na Wanyamapori 33

2.1.4. Ukiukwaji wa Sheria za Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori. 34
2.1.5. Ukosefu waRasilimali za Kutosha katika Kusimamia na Kuhifadhi Misitu na Wanyamapori. 34
2.1.6. Kutokuwepo kwa Mgawanyo Sawa wa Mapato kati ya Serikali na Wananchi 35
2.2. Maana na Aina za Migogoro katika Usimamizi wa Misitu Wanyamapori..... 35
2.2.1. Migogoro kati ya Wananchi na Mamlaka za Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori. 35
2.2.2. Migogoro Inayosababishwa na Baadhi ya Rasilimali za Maliasili kama Wanyama Kuvamia Mashamba ya Wananchi na Kuharibu Mazao..... 35
2.2.3. Migogoro ya Wananchi na Serikali kuhusu Mapato Yatokanayo na Misitu na Wanyamapori. 36
2.3. Athari za Migogoro katika Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori 36
2.3.1. Kudhoofika kwa Mchakato au Jitihada za Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori; 36
2.3.2. Kuharibika kwa rasilimali za Misitu na Wanyamapori ikiwa ni pamoja na kuharibiwa kwa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyapori. 36
2.3.3. Kutokea kwa Vifo na Kujeruhiwa kwa Baadhi ya Wananchi. 37

HITIMISHO 38

SHUKRANI

Mwongozo huu umewezeshwa kwa ufadhili wa Watu wa Marekani kupitia Shirika la Misaada la Maendeleo la Kimataifa la Marekani (USAID). Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT) inawajibika na yaliyomo. Yaliyomo katika mwongozo huu yasichukuliwe kuwa maoni ya USAID au Serikali ya Marekani.

Kukamilika kwa mwongozo huu ni matokeo ya ushiriki wa wadau kutoka taasisi mbalimbali. Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT) inapenda kutoa shukrani kwa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID) kwa kufadhili mradi huu ikiwa ni pamoja na kutoa msaada wa kitaalamu kupitia Mradi wa Kujengea Uwezo Kuleta Uwajibikaji (Pamoja Twajenga).

Shukranizakipekeeziendekwataasisizifuatazo:Wizaraya Maliasilina Utalii kupitia Wakala waHuduma za Misitu Tanzania(TFS), Shirika la World Wide Fund for Nature (WWF), ENVIROCARE, NEMC, Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), HAKIARDHI na Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF). Asasi hizi zilitoa wataalamu wake ambao walishiriki katika hatua mbalimbali za utayarishaji wa mwongozo huu.

Mwisho, LEAT inapenda kuwashukuru wajumbe wake wa bodi na wafanyakazi wote ambao walishiriki katika hatua mbalimbali za kufanikisha kazi hii.

Aidha, LEAT inawashukuru wote ambao walishiriki kwa namna moja au nyingine kuikamilisha kazi hii lakini hawakutajwa hapa.

DIBAJI

Mwongozo huu unalenga kutoa mafunzo kwa kada zote zinazohusika na usimamizi wa maliasili nchini kuanzia viongozi na wafanyakazi wa Serikali katika wizara, halmashauri, tarafa, kata, vijiji mpaka ngazi ya kaya.

Mwongozo huu unaainisha mambo muhimu yanayohusu ushiriki wa wananchi katika usimamizi wa misitu na wanyamapori. Mambo hayo ni pamoja na:

Dhana ya usimamizi wa maliasili nchini. Katika eneo hili mwongozo unafafanua maana ya maliasili, usimamizi wa maliasili za misitu na wanyamapori na malengo ya usimamizi.

Pia, mwongozo unaainisha njia mbalimbali za usimamizi wa misitu na wanyamapori, taasisi za usimamizi, sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayoelekeza ushiriki wa wananchi katika usimamizi wa rasilimali hizi.

Mwisho, mwongozo huu unataja changamoto zinazoikumba/kuikabili sekta ya maliasili hasa misitu na wanyamapori na kuainisha vyombo vinavyohusika na kupendekeza njia mbalimbali za kutatua migogoro.

Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT) inaamini kuwa mwongozo huu utasaidia kuleta mabadiliko chanya ya ushiriki wa wananchi katika usimamizi wa misitu na wanyamapori nchini.

UTANGULIZI

Tanzania ni nchi yenye rasilimali nyingi za maliasili na malikale ikiwemo misitu na wanyamapori. Kwa mujibu wa sheria za nchi, utajiri huu wa rasilimali humilikiwa na wananchi wote, Serikali ina dhamana ya kutunza na kuhifadhi maliasili hizi kwa niaba ya wananchi.

Tanzania ina ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 945,000. Kati ya hizo, takribani hekta milioni 48[1]ni misitu. Miongoni mwa hizo kiasi cha hekta milioni 13[2]ni hifadhi za maji na ardhi na uhaianuai[3]. Serikali ina dhamana ya kusimamia na kuhifadhi maliasili za wanyamapori ikiwa ni pamoja na kusimamia Hifadhi za Taifa, Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu. Mpaka sasa Serikali inasimamia Hifadhi za Taifa 16, Mapori ya Akiba 28, na Mapori Tengefu 44.

Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za misitu kupitia Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu (PFM). Misitu ni chanzo muhimu cha nishati, pamoja na umuhimu huo baadhi ya misitu iliyohifadhiwa na isiyohifadhiwa inaendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo uchomaji moto ovyo, utengenezaji mkaa, na ukataji miti uliokithiri kwa shughuli za kibinadamu. Changamoto hizi husababisha kukauka kwa vyanzo vya maji, kutoweka kwa uoto wa asili na kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Vilevile, Tanzania ni miongoni mwa mataifa machache duniani yenye utajiri mkubwa wa rasilimali za wanyamapori.Utajiri huu umesababisha kuanzishwa kwa hifadhi za wanyamapori. Pamoja na utajiri huu, Tanzania inakabiliwa na changamoto mbalimbali za kuhifadhi na kutunza wanyamapori kama vile ujangili uliokithiri hasa kwa Tembo na Faru unaosababishwa na kuongezeka kwa kukua kwa biashara ya pembe za wanyama hao katika mataifa ya Mashariki ya Mbali. Wanyama wengine kama vile Swala na Nyati wameendelea kukumbwa na tatizo la ujangili kutokana na mahitaji mbalimbali ya binadamu.

Katika kuhakikisha kuwa rasilimali za misitu na wanyamapori zinalindwa na kuhifadhiwa, Tanzania imetunga sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali lakini utekelezaji duni wa sheria umebaki kuwa kikwazo kikubwa cha kuweka na kuleta usimamizi mzuri katika sekta ya maliasili. Katika Kutimiza azma ya ushirikishwaji wa wananchi katika usimamizi wa wanyamapori, Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) 38 zimesajiliwa, kati ya hizo 19[4] zimeidhinishwa kutumia rasilimali za wanyamapori.

Hata hivyo ni vyema kutambua kuwa changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika ushiriki wa wananchi katika usimamizi wa rasilimali za misitu na wanyamapori nchini zinaweza kutofautiana kutoka eneo moja la nchi hadi lingine.

Hivyo basi mwongozo huu utawawezesha wananchi kuelewa vyombo vya usimamiziwa maliasili, sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali kuhusu sekta za misitu na wanyamapori pamoja na kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazoikabili sekta hii.

---

1 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), 2013.
2 Wakala Wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), 2013
3 Wakala Wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), 2013
4 Hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Bunge la Bajeti Mwaka 2013/2014

USIMAMIZI

SURA YA KWANZA
USIMAMIZI WA MALIASILI ZA MISITU NA WANYAMAPORI

1.0. Utangulizi

Sura hii inaelezea maana ya maliasili na kufafanua kwa kina dhana ya usimamizi wa maliasili ikiwa ni pamoja na kuangalia ushiriki wa wananchi katika usimamizi wa maliasili za misitu na wanyamapori.

1.1. Maliasili ni nini?

Maliasili ni rasilimali za asili kama vile misitu na wanyama zinazopatikana katika nchi. Maliasili ni rasilimali muhimu kwa taifa lolote kutokana na mchango wake muhimu katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni, na kimazingira. Pamoja na misitu na wanyamapori, rasilimali hizo zinajumuisha ardhi, madini, mito, maziwa na bahari, gesi asilia na makaa ya mawe[5].

1.2. Usimamizi wa Maliasili

Usimamizi wa maliasili unalenga kuhakikisha kuwa kuna uhusiano endelevu kati ya watu na rasilimali zao. Usimamizi unajumuisha mipango na hatua mbalimbali zihusuzo matumizi ya ardhi, usimamizi wa maji, uhifadhi wa uhaianuai na uendelezaji wa shughuli za sekta za kilimo, madini, utalii, uvuvi na misitu. Usimamizi wa rasilimali ni hatua muhimu katika kuhakikisha kuwa rasilimali za asili zinatumika kwa tija na zinanufaisha kizazi cha sasa na vijavyo.

Jukumu kuu la usimamiziwa rasilimali za misitu na wanyamapori nchini limepewa Wizara ya Maliasili na Utalii kwani rasilimali hizi zimetamkwa na sheria kuwa ni mali ya taifa kupitia Wizara hii. Kwa maana hiyo, serikali ndiye msimamizi mkuu. Licha ya serikali kupewa jukumu la usimamizi, zipo taasisi za kiutafiti ambazo hutoa mbinu elekezi za usimamizi wa wanyamapori na misitu na kuchangia uboreshaji wa usimamizi rasilimali hizi nchini.

Hata hivyo, kwa kuwa rasilimali hizi ni mali ya wananchi, kila mwananchi ana jukumu la kuhakikisha kuwa anashiriki kikamilifu katika kupanga, kumudu, kutunza, kuhifadhi na kuhamasisha juu ya matumizi endelevu ya maliasili nchini. Jukumu hili kubwa ni la kila mwananchi kwa mujibu wa Ibara ya 27(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

1.3. Malengo ya Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori

Malengo ya jumla ya usimamiziwa misitu na wanyamapori ni pamoja na:

- Kuhifadhi makazi asilia ya nchi kavu na majini pamoja na viumbe vyake;
- Kuhifadhi idadi ya kutosha ya viumbe, huku mkazo ukiwekwa kwa wanyama walio hatarini kutoweka;
- Kulinda maeneo yenye mandhari nzuri na yenye mvuto na umuhimu kwa uchumi kama vile milima, mabonde, mito maziwa na kadhalika; na
- Kuhifadhi vyanzo vya maji.

1.4. Faida za Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori:

Usimamizi wa maliasili za misitu na wanyamapori una faida mbalimbali baadhi ya faida hizo ni:

- Kutoa fursa na mazingira yanayofaa kwa watu kutumia maliasili za misitu na wanyamapori katika kuleta maendeleo;
- Kuchangia pato la Taifa kutokana na fedha za kigeni zinazotokana na shughuli za utalii;
- Ni njia thabiti ya kulinda Taifa dhidi ya athari za mabadiliko ya tabia nchi;
- Misitu huifadhi vyanzo vya maji;
- Misitu na Wanyamapori ni chanzo cha ajira kwa wananchi;
- Misitu hutoa dawa mbalimbali kwa matumizi ya binadamu, mimea na wanyama; na
- Wanyamapori na misitu ni sehemu ya uhainuwai ambao huleta mlingano mzuri wa mimea, viumbe na mazingira.

NJIA ZA USIMAMIZI WA MISITU NA WANYAMAPORI

2.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha njia mbalimbali zinazotumika katika usimamizi wa rasilimali za misitu na wanyamapori ikiwa ni pamoja na usimamizi kwa amri na udhibiti, usimamizi wa kijamii, usimamizi wa mazoea na usimamizi wa kuji hadhari. Lengo la sura hii ni kumwezesha mwananchi kuelewa njia hizi ambazo hutumika katika usimamizi wa misitu na wanyamapori.

2.1 Njia za Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori

Njia mbali mbali za usimamiziwa maliasili za misitu na wanyamapori ni pamoja na:

- Mfumo wa kushurutishaamrisha (Top down Approach)
- Usimamizi wa maliasili wa kijamii (CBNRM)
- Usimamizi wa mabadiliko-mnyumbuko (Adaptive management)
- Usimamizi wa kujihadhari(Precautionary approach)
- Usimamizi wa Maliasili Jumuishi (Integrated natural resource management)

2.1.1 Usimamizi wa Kuamrisha / kushurutisha?

Hii ni njia mojawapo ya usimamizi wa maliasili inayozingatia utekelezaji wa maamuzi na mapendekezo kutoka ngazi ya juu ya utawala kwenda ngazi ya chini. Katika njia hii mamlaka za juu za kiutawala hutoa maagizo kwa mamlaka za chini juu ya utekelezaji wa mambo mbalimbali yanayohusu usimamizi wa maliasili. Njia hii imejikita katika kuhakikisha kuwa taasisi za chini za kiutawala zinakuwa watekelezaji wa maagizo au maelekezo kutoka taasisi za juu bila kuwa na nafasi ya kushiriki katika kufikia maamuzi hayo au kutoa mapendekezo yanayoendana na mazingira ya eneo husika.

2.1.2 Usimamizi wa Maliasili wa Kijamii

Usimamiziwa maliasili wa kijamii hujumuisha malengo ya uhifadhi na upatikanaji wa faida za kiuchumi kwa jamii za vijijini na maeneo yaliyo karibu na hifadhi mbalimbali. Falsafa kuu tatu zinazotetea usimamiziwa namna hii ni:

- kwanza, jamii za vijijini zina nafasi nzuri za kusimamia rasilimali;
- pili, jamii itasimamia rasilimali ikiwa manufaa ni makubwa kuliko gharama ya uhifadhi na
- tatu, jamii zitasimamia rasilimali pindi rasilimali hizo zina uhusiano wa moja kwa moja na ubora wa maisha yao.

Usimamizi huu unalenga kutoa mamlaka na haki kamili kwa taasisi za ngazi za chini kabisa katika kusimamia maliasili kama vile misitu, wanyamapori, ardhi, maji na nyinginezo.

2.1.3 Usimamizi wa Mabadiliko-Mnyumbuko (Adaptive management)

Njia hii ya usimamiziwa maliasili inalenga kutambua na kuhimili matatizo kulingana na hali halisi. Aina hii ya usimamizi huzingatia uzoefu na taarifa mbalimbali za usimamizi wa maliasili katika eneo husika. Mfumo huu wa

usimamizi huwezesha watu husika kuchukua hatua zifaazo kuleta usimamizi bora wa maliasili kutokana na uzoefu na changamoto walizozipata katika harakati zao za kumudu rasilimali husika.

2.1.4 Usimamizi wa Maliasili Jumuishi/Mkamilifu;

Usimamizi wa Maliasili Jumuishi/Mkamilifu ni njia mojawapo ya usimamizi unaojumuisha namna kadhaa za matumizi ya maliasili kama vile matumizi ya kibaiolojia, kisiasa, kijamii na kiuchumi ili kufikia malengo ya watu mbalimbali katika jamii. Aina hii ya usimamizi huunganisha wadau wote kuanzia ngazi ya mipango mpaka utekelezaji ili kupunguza uwezekano wa mifarakano. Ushirishaji huwezesha wadau wote kujiona ni wanahisa katika maliasili husika na hivyo kutoa mchango wao mkamilifu katika kuimudu kwa manufaa yao na wadau wengine.

TAASISI ZA USIMAMIZI WA MISITU NA WANYAMAPORI

3.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea taasisi mbalimbali za usimamiziwa misitu na wanyamapori. Inafafanua kwa ufupi kazi na wajibu wa mamlaka hizo. Ili kufanikisha usimamizi madhubuti wa rasilimali za misitu na wanyamapori nchini taasisi hizi ni vyema zikashirikiana kikamilifu.

3.1 Taasisi za Usimamizi wa Misitu Tanzania

Mpangilio wa kitaasisi wa usimamizi wa misitu umegawanywa katika sehemu kuu tatu ambazo ni Serikali kuu, Serikali za Mitaa, na Serikali za Vijiji.

Serikali Kuu

- Misitu yote ya hifadhi ya taifa husimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu(TFS) chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Huduma za Misitu ana mamlaka ya kusimamia, kufuatilia na kukagua usimamizi wa hifadhi ya misitu ya taifa.
- Waziri mwenye dhamana ya misitu ana jukumu la kuhakikisha kuwa maafisa au watumishi wa Serikali wanaosimamia sheria wanatekeleza majukumu yao.
- Mtendaji mkuu wa Wakala wa Huduma za Misitu ana jukumu la kuishauri Serikali katika masuala yote yanayohusiana na utunzaji na usimamizi wa misitu.
- Maafisa mbalimbali walioteuliwa wana jukumu la kuhakikisha uwepo wa usimamizi bora wa misitu na matumizi yenye tija.

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ilianzishwa kisheria tarehe 1 Julai 2010 chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali namba 9 ya mwaka 1997 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2009. Wakala wa Huduma za Misitu ilianza kufanya kazi rasmi tarehe 1 Julai 2011. Wakala imechukua shughuli za kiutendaji ambazo zilikuwa zinatekelezwa na Idara ya Misitu na Nyuki chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania katika kutekeleza mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) pamoja na Sera ya Misitu ambayo inasisitiza katika kuhakikisha matumizi endelevu ya misitu, imefanya maboresho katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha kuwa mapato ya Serikali yanaongezeka na kuongeza udhibiti wa uvunaji na ukusanyaji wa mapato. Maeneo yaliyofanyiwa maboresho ni pamoja na:

- Kufanya mapitio ya bei ya mazao ya Misitu;
- Kufanya mapitio ya Mwongozo wa Uvunaji Endelevu wa Misitu wa Mwaka 2007;
- Uuzaji wa miti ya Misaji (Teak) kwa njia ya mnada; na
- Kuimarisha ulinzi katika vizuizina kusitisha ukusanyaji wa maduhuli katika vizuizi hivyo.

Serikali za Mitaa
Misitu ya hifadhi ya Serikali za Mitaa husimamiwa na serikali za mitaa kupitia maafisa misitu wa Halmashauri za Wilaya.

Serikali za Vijiji.
Misitu ya hifadhi ya vijiji inasimamiwa na serikali za vijiji kupitia Kamati za Maliasili za Vijiji.

Wananchi
Wananchi kupitia Serikali za Vijiji ni taasisi nyingine muhimu katika usimamizi wa rasilimali za misitu. Jukumu la usimamizi wa misitu ni la wananchi wote na ni suala la kikatiba kwani Ibara ya 27(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa jukumu kwa kila mwananchi kulinda rasilimali za nchi yetu na kuhakikisha zinatumiwa kwa njia iletayo manufaa kwa nchi nzima.

3.2.1 Taasisi za Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania

Wizara ya Maliasili na Utalii
Hii ni wizara yenye dhamana na jukumu la kusimamia maliasili, malikale na shughuli zote za kitalii nchini. Wizara hii husimamia taasisi, wakala na idara mbalimbali katika kutekeleza majukumu yahusuyo uhifadhi, matumizi endelevu ya maliasili na maendeleo ya utalii.
Shughuli za wizara zinazohusiana na usimamizi wa wanyamapori ni pamoja na:

- Kutengeneza na kupitia kanuni mbalimbali zihusuzo usimamizi wa wanyamapori;

- Kusimamia utalii na uwindaji wa wanyamapori;
- Kuboresha huduma, miundombinu na vitendea kazi;
- Kushirikiana na mashirika mbalimbali katika utekelezaji wa miradi ya usimamizi wa wanyamapori;
- Kusimamia taasisi na idara za serikali zikiwemo: Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori Tanzania, Idara ya Wanyamapori, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania, Shirika la Hifadhi za Taifa, na Vyuo vya Taaaluma ya Wanyamapori.

Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)

Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) ilianzishwa na Sheria ya TANAPA ya Mwaka 1959. Mamlaka hii husimamia Hifadhi za Taifa zote.

Mamlaka ya Hifadhi za Taifa hufanya shughuli zifuatazo:

- Kumudu, kusimamia,na kuratibu shughuli za kitalii ndani ya mipaka ya Hifadhi za Taifa kama chanzo kikuu cha mapato;
- Kufanya doria ndani ya mipaka ya Hifadhi za Taifa;
- Kutatua migogoro ya mipaka;
- Kuboresha miundombinu ya majengo, madaraja, barabara, nyumba za wafanyakazi, huduma ya maji, na umemejua;
- Kuimarisha utalii na kupanua wigo wa vivutio na huduma kwa watalii;
- Kuimarisha uhifadhi;
- Kuendesha miradi inayoshirikisha wananchi kuzunguka maeneo ya hifadhi ikiwa ni pamoja na kuendesha miradi ya ujirani mwema.

Idara ya wanyamapori

Shughuli zinazofanywa na Idara ya Wanyamapori ni pamoja na:

- Kulinda wanyamapori na makazi yote asilia nje ya mipaka ya Hifadhi za Taifa na Hifadhi ya Ngorongoro;
- Kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu na uhifadhi wa wanyamapori;
- Kusimamia shughuli zote za uwindaji zinazofanyika ndani ya Mapori ya Akiba naMapori Tengefu.

Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ilianzishwa kwa Sheria ya Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro ya Mwaka 1959.

- Mamlaka ya Ngorongoro hulinda rasilimali pamoja na jamii ya kimasai inayoishi katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro;
- Mamlaka husimamia shughuli zote za uhifadhi na za kijamii ndani ya mipaka ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro;
- Pamoja na shughuli nyingine Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro huhusika na ufanyaji doria ndani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro;
- Pia mamlaka huchangia katika utekelezaji wa miradi ya ujirani mwema.

SEHEMU YA PILI

SERA, SHERIA NA KANUNI ZINAZOHUSIANA NA MALIASILI

SURA YA KWANZA

SERA ZINAZOHUSU USIMAMIZI WA MISITU NA WANYAMAPORI

1.0 Utangulizi

Mfumo wa usimamizi wa misitu na wanyamapori nchini umepitia katika vipindi tofauti tofauti vyenye mabadiliko mbalimbali. Sera na sheria za usimamizi wa maliasili za misitu, wanyamapori, maji na rasilimali nyingine zilianzishwa na mamlaka za kikoloni kabla ya uhuru. Katika kipindi cha ukoloni sheria nyingi za usimamizi zililenga kuondoa mamlaka ya usimamizi wa maliasili kutoka kwa wananchi na kuipa serikali ya kikoloni jukumu hilo. Kwa sehemu kubwa sheria hizi ziliondoa haki ya wananchi kunufaika moja kwa moja na maliasili hizo.

Baadhi ya sheria nyingi zilizotungwa baada ya uhuru zilirithi mfumo wa kikoloni katika kusimamia maliasili. Kwa sasa sheria nyingi za usimamiziwa maliasili zinataja kuwa Raisi ndiye mwenye dhamana ya usimamizi nchini kwa niaba ya wananchi.

Sura hii inaainisha sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayohusu usimamizi wa misitu na wanyamapori. Inaeleza kwa ufupi namna ambavyo sera na sheria hizi muhimu katika usimamizi na jinsi ambavyo zinategemeana katika usimamizi wa misitu na wanyamapori.

1.1 Sera ni nini?

Sera ni tamko linalotoa dira au mwelekeo wa kufanikisha jambo lililokusudiwa na linalokusudiwa. Sera hutoa mwongozo wenye lengo la kufafanua dhima na malengo ya jambo ikiwa ni pamoja na kuainisha shughuli zitakavyoendeshwa na kusimamiwa pamoja na kufafanua jinsi wadau mbalimbali watakavyoshirikishwa katika jambo hilo.

1.1. Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998

Sera ya Taifa ya Misitu inaainisha maeneo matatu ya kipaumbele kwa ajili ya sheria na utekelezaji, yaani:

- Usimamizi wa misitu na mazao;
- Utunzaji na usimamizi wa ikolojia;
- Taasisi na rasilimali watu.

Sera inatoa wito na kuhamasisha jamii katika usimamizi shirikishi wa misitu. Hii inafanyika kwa njia ya kuanzisha mfumo wa usimamizi wa pamoja wa misitu ya hifadhi (Joint Forest Management (JFM)) na usimamizi wa jamii wa misitu nje ya hifadhi (Participatory Forestry Management (PFM)). Lengo la usimamizi shirikishi wa misitu ni kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya usimamizi na maendeleo ya sekta ya misitu na mgawanyo wa majukumu kati ya jamii na Halmashauri za Wilaya. Inaongeza nafasi kwa ajili ya ushiriki mpana wa watu katika usimamizi wa misitu na mazao yake.

1.2. Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997

Sera inatambua kuwa maisha ya binadamu yanategemea mazingira na hivyo kila mwananchi ana jukumu la kushiriki kikamilifu katika kutunza na kuhifadhi mazingira. Sera hii inataja matatizo sita ya mazingira ambayo yanahitaji ufumbuzi. Matatizo haya ni pamoja na:

- Uharibifu wa ardhi;
- Uhaba wa maji safi na salama kwa wakazi wa mijini na vijijini;
- Uchafuzi wa mazingira;
- Upotevu wa makazi ya wanyamapori na uhainuwai;
- Uharibifu wa mazingira na kudhoofika kwa viumbe wa majini; na
- Ukataji miti ovyo.

Pia, sera inataja sababu nyingine zinazoharibu mazingira ambazo ni ongezeko la watu vijijini na mijini nausimamizi duni wa ardhi na maji katika maeneo mbalimbali ya Tanzania.

Tamko namba 33 la Sera hii linafafanua kuwa sera ya mazingira, mipango na mikakati yake inaweza kuleta manufaa yanayostahili iwapo tu itaoanishwa na kuwianishwa na sera nyingine za kitaifa. Hivyo basi sera za kisekta, pamoja na -mipango- mikakati - yake lazima zioanishwe na sera, mikakati na mipango ya usimamizi mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali.

Pamoja na mambo mengine, Sera ya Taifa ya Mazingira inazitaka Serikali za Mitaa kuwajibika kikamilifu katika usimamizi wa mazingira. Pia, inatoa mamlaka kwao kusimamia michakato na mipango ya uanzishwaji wa miongozo na kanuni za mazingira ikiwa ni pamoja na kuunda Kamati za Mazingira chini ya uongozi na usimamizi wa Halmashauri za Wilaya, Kata, na Vijiji.

1.3. Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995

Sera ya Taifa ya Ardhi inaainisha mambo makuu yafuatayo:

- Ardhi ni mali ya umma na iko chini ya Raisi kama mdhamini kwa niaba ya watanzania;
- Ardhi ina thamani;
- Wananchi wanapaswa kulipwa fidia stahiki kwa muda muafaka pale ambapo ardhi yao inapotwaliwa;
- Wananchi wote, wake kwa waume, wana haki sawa ya kupata na kumiliki na kurithi ardhi;
- Ardhi itatumika kwa namna ambayo inaleta manufaa kwa maisha ya watanzania; pamoja na,
- Kuweka mfumo bora wa matumizi ya ardhi na njia mbalimbali za utatuzi au usuluhishi wa migogoro ya ardhi.

SEHEMU YA PILI

SHERIA ZINAZOHUSU USIMAMIZI WA MISITU NA WANYAMAPORI

2.0 Sheria ni nini?

Sheria ni mfumo wa kanuni unaotoa mwongozo wa jinsi ya kufanya mambo kwa usahihi. Sheria lazima zifuatwe na watu wote, na anayekiuka sheria huadhibiwa. Chombo chenye mamlaka ya kutunga sheria nchini ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria.

Sheria za sekta ya misitu na wanyamapori zinaeleza juu ya udhibiti na usimamizi wa rasilimali za misitu na wanyamapori kupitia mamlaka ya serikali kuu na serikali za mitaa.

Sura hii inachambua sheria zinazohusu usimamiziwa misitu na wanyamapori ili kuwezesha wananchi kufahamu na kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

2.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Namba 2 ya Mwaka 1977

Katiba ni sheria mama inayotoa mwongozo na utaratibu juu ya namna ambavyo mamlaka za nchi zinatakiwa kulinda na kusimamia maliasili za nchi. Falsafa ya usimamizi na uhifadhi wa maliasili nchini inapata uhalali kutoka katika katiba hii kwani Ibara ya 27(1) na (2) inatoa wajibu kwa kila mtanzania kulinda maliasili za nchi, mali ya mamlaka ya nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi, na pia kuiheshimu mali ya mtu mwingine.

Katiba pia inafafanua kuwa watu wote kwa mujibu wa sheria wanapaswa kutunza maliasili, kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Taifa kwa makini kwa kuzingatia ukweli kwamba wao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya Taifa lao. Hili ni jukumu takatifu? na ambalo ni lazima litekelezwe kikamilifu na kila mwananchi.

> ***Zingatia:***
> Suala la usimamizi wa maliasili ni jukumu la kila mwananchi hivyo kila mmoja anapaswa kuhakikisha kuwa anashiriki kikamilifu katika kusimamia rasilimali za misitu na wanyamapori kwa mujibu wa sheria na kwa masilahi ya umma.

2.2 Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999

Sheria ya Ardhi inagawanya ardhi katika makundi makuu matatu ambayo ni:

- Ardhi ya Jumla;
- Ardhi ya Hifadhi;
- Ardhi ya Vijiji.

Ardhi ya Jumla ni ardhi ya umma ambayo si ardhi ya hifadhi wala ardhi ya kijiji. Kwa ufupi hii ni ardhi ambayo iko chini ya umiliki au usimamizi na usimamizi wa Kamishina wa Ardhi. Watu wengi wenye kumiliki ardhi mijini na wenye hati zilizotolewa na Kamishina wa Ardhi humiliki ardhi ya jumla. Hii ni sehemu ndogo sana ya ardhi ya nchi yetu kwani ardhi hii ni asilimia mbili tu ya ardhi ya nchi yetu.

Ardhi ya Hifadhi ni ardhi ambayo imetengwa kwa ajili ya hifadhi za taifa kama hifadhi za wanyamapori na hifadhi za misitu, barabara, hifadhi za kimazingira au ardhi hatarishi. Ardhi iliyo katika fungu hili inasimamiwa na sheria ya hifadhi husika. Kwa mfano, Sheria ya Hifadhi za Wanyamapori na Sheria ya Misitu, na Sheria ya Barabara kutaja chache kati ya nyingi.

Ardhi ya vijiji ni ardhi ambayo iko ndani ya mipaka ya kijiji na imesajiliwa kisheria kuwa ndani ya mipaka ya kijiji. Ardhi ya Vijiji ni asilimia 70 ya ardhi yote ya nchi yetu. Mamlaka ya usimamizi wa ardhi ya kijiji iko chini ya Halmashauri ya kijiji (Serikali ya Kijiji). Ardhi ya vijiji inasimamiwa na sheria ya Ardhi Namba 5 ya Mwaka 1999 au Sura ya 114 ya Toleo Lilorejewa la Mwaka 2002. Ni vema kwa serikali za vijiji na wanavjiji kuielewa sheria hii na sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ili kuweza kulinda na kusimamia vyema ardhi iliyoko katika mamlaka yao.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999 chini ya kifungu cha 181, kama kuna mkanganyiko wa sheria yoyote kuhusu mambo muhimu yanayohusu ardhi, basi Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999 itatumika.

2.3 Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999

Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999 inaelezea usimamizi wa ardhi ya vijiji. Pia, inaelezea umiliki wa ardhi katika ardhi ya kijiji pamoja na rasilimali za misitu na wanyamapori zilizopo katika vijiji. Sheria hii inatoa mamlaka kwa Halmashauri za Vijiji kusimamia ardhi kwa niaba ya wanakijiji ndani ya kijiji husika.

Katika kusimamia ardhi ya kijiji, Halmashauri za Vijiji zinatakiwa kuzingatia falsafa ya matumizi endelevu kupitia uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kuepusha migogoro katika matumizi ya rasilimali. Halmashauri za Vijiji zinatakiwa kushauriana na Halmashauri za Wilaya, ambazo zina mamlaka katika eneo hilo, ili kuweka utaratibu wa kisheria katika kutatua migogoro ya ardhi.

2.4 Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Namba 7 ya Mwaka 1982

Sheria hii inatoa mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana kuanzisha Halmashauri za Wilaya, Miji na Vijiji. Sheria hii inazitambua Halmashauri za vijiji kuwa ni serikali katika vijiji ambazo ziko chini ya Mkutano Mkuu wa Vijiji. Hivyo hizi ni serikali na zinajukumu la kuleta maendeleo kwa wanavijiji wao. Serikali hizi zimepewa madaraka ya kutunga sheria ndogondogo ambazo ni lazima zipitishwe na mkutano mkuu wa kijiji husika na kukubaliwa (kuridhiwa) na Halimashauri ya Wilaya ili kuhakikisha kuwa mahitaji yote yaliyoelezwa na sheria yamezingatiwa ikiwemo kikomo cha faini.

Sheria hii inasisitiza uwepo wa Mkutano Mkuu wa Kijiji kama mamlaka ya juu kabisa katika masuala yote yanayohusu utungaji wa sheria ndogondogo na miongozo mbalimbali ya uendeshaji wa vijiji. Halmashauri ya kijiji itahusika na masuala yote ya kiutendaji katika uendeshaji wa shughuli za kijiji. Moja ya kazi za serikali ya kijiji ni kupanga na kuratibu shughuli za maendeleo ikiwemo kushiriki katika shughuli za usimamizi wa misitu na wanyamapori. Sheria hii inatoa nguvu ya usimamizi wa misitu kwa kamati ya kudumu ya uchumi, kazi na mazingira ya Halmashauri za Wilaya.

2.5 Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Namba 8 ya Mwaka 1982

Sheria hii inaeleza uwezo wa kutunga sheria na kuanzishwa kwa mamlaka za serikali za mitaa (Mamlaka za Miji) zilizopo chini ya mamlaka ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya serikali za mitaa.

Sheria hii inaeleza uhusiano uliopo kati ya mamlaka ya serikali za mitaa na serikali kuu. Serikali kuu inatakiwa kutambua uhuru wa serikali za mitaa. Madaraka na majukumu ya mamlaka ya miji kama ilivyoelezwa katika sheria hii, zina athari juu ya usimamizi wa misitu, wanyamapori na rasilimali zingine. Kwa mfano, vifungu vya 5, 94, na 95 vya nyongeza ya Sheria hii vinarejea shughuli zinazohusiana na misitu.

2.6 Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 20 ya Mwaka 2004

Hii ni sheria mama inayoshugulikia usimamizi wa masuala yote ya mazingira nchini. Mazingira ni suala mtambuka katika sekta zote zinazohusiana na usimamizi na matumizi ya rasilimali. Sheria hii inatoa utaratibu wa kisheria na kitaasisi kwa ajili ya usimamizi endelevu wa mazingira.

Sheria inatoa utaratibu wa kushughulikia migogoro inayotokana na usimamizi wa rasilimali za mazingira zinazohusu sekta mbalimbali. Kwa kuzingatia hili, kifungu cha 30 cha sheria hii kinataka uanzishwaji wa Kitengo cha Mazingira katika kila wizara na taasisi za serikali zenye kuhusika na sekta mbalimbali za kimazingira.

Waratibu katika kitengo hicho wanatakiwa kuwa kiungo kati ya wizara au taasisi zao na ofisi ya Makamu wa Rais. Miongoni mwa majukumu yao ni kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na ya Wizara husika juu ya utekelezaji wa majukumu yao.

Waziri wa Tawala za Mikoa anatakiwa kuteua wataalamu wa usimamizi wa mazingira wa mkoa kuzishauri serikali za mitaa juu ya utekelezaji na uzingatiaji wa sheria hii na zile zihusuzo sekta mbalimbali za mazingira. Wataalamu hawa wanatakiwa kuwa kiungo muhimu kati ya mikoa na Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC.

Mamlaka za serikali za mitaa yaani, Halmashauri za Wilaya na Miji zinatakiwa kuteua maafisa wa usimamizi wa mazingira. Majukumu ya maafisa hawa ni pamoja na kutoa ushauri kwa kamati za usimamizi wa mazingira, kuandaa taarifa mara kwa mara juu ya utekelezaji wa masuala ya mazingira, kurekebisha sheria ndogo ndogo juu ya usimamizi wa mazingira na shughuli zote kuhusiana na mazingira katika kila sekta. Sheria hii inataka utunzaji na usimamizi wa mazingira uwe endelevu na uzingatie kanuni za kimataifa za utunzaji mazingira kama vile kanuni za: hatua za kinga na tahadhari; mchafuzi alipe, uchambuzi wa mguso/athari za kimazingira; uwiano wa haki wa kizazi cha sasa na kijacho, maendeleo endelevu; haki ya kupata habari na haki za kimazingira; na jaliwa? moja lakini majukumu tofauti.

Sheria ya Mazingira inaeleza kwa uwazi kuwa kama sheria yoyote inapingana na sheria hii kuhusu suala lolote la usimamizi wa mazingira, basi sheria hiyo itakuwa batili kwa kiwango cha upingaji au kutofautiana kwake.

2.7 Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002

Hii ndiyo sheria mama inayotoa utaratibu mzima wausimamizi wa misitu nchini. Sheria hii inalenga kuimarisha utawala bora wa misitu katika ngazi ya jamii ili kuondokana na dhana ya maagizo na kuamrisha katika jitihada za kutekeleza Sera ya Misitu ya Mwaka 1998 na dhana ya madaraka kwa Serikali za Mitaa.

Kifungu cha 22(1) cha sheria hii kinampa Waziri ahusikaye na misitu, kutangaza katika Gazeti la Serikali eneo lolote lenye viumbe hai kuwa mamlaka ya hifadhi za misitu. Sheria inataja kanuni mbalimbali zitumikazo katika kutunza na kusimamia misitu na inatilia mkazo ufanywaji wa uchambuzi wa mguso/athari za mazingira kwa miradi yoyote ile katika maeneo ya misitu. Misitu inatajwa kuwa ni rasilimali ya taifa ambayo iko chini ya Wizara na kuwa uvunaji wake lazima uwe kwa mujibu wa leseni na vibali husika.

2.8 Sheria zinasosimamia Wanyamapori Tanzania

2.8.1 Sheria ya Hifadhi za Taifa ya Mwaka 1959

Sheria hii ndiyo sheria mama inayotoa utaratibu wa namna Hifadhi za Taifa zitakavyoanzishwa na kusimamiwa. Rais anapewa mamlaka na kifungu cha 3 cha sheria hii kutangaza eneo lolote nchini kuwa Hifadhi ya Taifa baada ya kupata ruhusa ya Bunge. Kwa mfano, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ilianzishwa chini ya kifungu cha 5 cha sheria na kwa sasa iko chini ya usimamizi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) ambalo ndicho chombo kikuu cha kiutendaji katika usimamizi wa Hifadhi za Taifa.

Pia, sheria hii inahakikisha kuwa falsafa nzima ya uanzishwaji wa hifadhi za taifa za wanyamapori inazingatiwa na imejikita katika kutenga maeneo na kuzuia makazi ya watu ndani ya hifadhi za taifa. Sheria hii huhakikisha uendelevu wa wanyamapori kama urithi wa watu wa Tanzania na ulimwengu mzima.

2.8.2 Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009

Sheria hii ilitungwa ilikuweka masharti ya uhifadhi, usimamizi na matumizi endelevu ya wanyamapori na mazao ya wanyamapori.

Maana ya "Hifadhi"inayotolewa katika sheria hii inajumuisha wanyamapori, makazi yao pamoja na mazingira kwa ajili ya ustawi wa viumbe hai.

Sheria inaainisha majukumu ya wananchi katika maeneo ya usimamizi wa wanyamapori, kuanzishwa kwa maeneo ya hifadhi katika ardhi ya vijiji (WMA), kutambua uhusiano muhimu kati ya wanyamapori na rasilimali za misitu na haja ya kushirikiana na kuratibu katika kuhakikisha matumizi endelevu ya misitu na wanyamapori.

Kifungu cha 31(6) cha sheria kinaeleza kwamba shughuli zitakazotekelezwa katika maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori lazima ziendane na Sheria za Misitu, Ufugaji Nyuki, Uvuvi na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Kama ilivyo kwa sheria za misitu, rasilimali zote za wanyamapori zilizopo katika hifadhi za taifa huhifadhiwa na kusimamiwa chini ya Sheria ya Hifadhi za Taifa na Shirika la Hifadhi la Taifa Tanzania (TANAPA). Inabidi ieleweke kuwa Serikali za Vijiji zina chaguo la kuanzisha na kusimamia misitu yao kwa mujibu wa sheria hii au kwa mujibu wa Sheria za Ardhi ya Vijiji ya Mwaka 1999, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Wilaya) ya Mwaka 1982, na Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 2007. Suala la kuzingatiwa ni kuwa usimamizi wa misitu na matumizi yake lazima uzingatie kanuni za utunzaji na usimamizi mazingira ikiwa ni pamoja na ile ya maendeleo endelevu.

KANUNI, MIONGOZO NA ADHABU

3.0 Kanuni ni nini?

Kanuni ni taratibu zinazotungwa na wizara au vyombo vingine vyenye mamlaka hayo kisheria. Kanuni hutungwa ili kutoa ufafanuzi wa mambo ambayo si rahisi kuyaelezea yote katika sheria kwa mfano: adhabu, tozo, utaratibu wa uvunaji wa misitu, utaratibu wa uanzishwaji wa Jumuiya za Uhifadhi wa Wanyamapori, na mambo mengine. Nchini Tanzania karibu sheria zote hutungiwa kanuni za kuelekeza namna zitakavyotumika au kufafanua na kuainisha kwa upana wake matakwa ya sheria na kutoa taratibu za kufuata katika kutekeleza sheria husika.

3.1 Miongozo

Miongozo ni taarifa elekezi zinazolenga kutoa ufafanuzi kuhusu namna jambo fulani linavyopaswa kutekelezwa. Nchini Tanzania miongozo mbalimbali huandaliwa na Serikali kuu katika sekta za misitu na wanyamapori juu ya utaratibu wa maombi ya uvunaji endelevu, njia za kuanzisha misitu na maeneo ya wanyamapori pamoja na mambo mengine mbalimbali.

3.1.1 Mwongozo wa Uvunaji a Endelevu wa Misitu wa Mwaka 2007

Mwongozo huu ni matokeo ya Sera ya Misitu ya Mwaka 1998 na Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002. Ili uvunaji uwe endelevu, kila mahali nchini, sharti kuwe na Mpango wa Usimamizi wa Misitu (Management Plan). Mwongozo unataja vyombo vyenye mamlaka ya kujadili na kupitisha maombi ya uvunaji, masharti ya biashara ya mazao ya misitu ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kuainisha nyaraka mbalimbali muhimu katika biashara ya mazao ya Misitu. Pia unaainisha tozo mbalimbali zihusuzo mazao ya misitu.

Vilevile, Mwongozo huu unaelekeza jinsi serikali za vijiji zitakavyotekeleza majukumu yake katika usimamizi na uvunaji wa misitu. Pamoja na mwongozo huu bado zipo changamoto mbalimbali zinazokwamisha ushiriki wa wananchi kama inavyoelezwa katika sehemu ya tatu ya mwongozo huu.

3.1.2 Kanuni za Uanzishwaji wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Mwaka 2012.

Kanuni za Hifadhi za Jumuiya za Wanyamapori zimeanzishwa chini ya Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009. Kanuni hizi zinafafanua maana ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA) kuwa ni “Ni ardhi ya kijiji iliyotengwa maalumu kwa hifadhi ya wanyamapori” kwa maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Kijiji. Kanuni hizi zinaelekeza utaratibu wa kuanzisha maeneo ya hifadhi za wanyamapori kwenye ardhi ya kijiji. Pia kanuni hizi zinataja malengo ya kuanzisha WMA ambayo ni pamoja na kusaidia jamii zinazoishi ndani ya kijiji kushiriki katika ulinzi na matumizi ya rasilimali za wanyamapori katika ardhi ya kijiji.

3.2 Makosa na adhabu katika sheria za Misitu

Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002 imeainisha makosa na adhabu mbalimbali.

- Kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002, ni kosa kwa mtu yeyote yule asiye na kibali au ruhusa kuingia katika hifadhi ya msitu, kutenda tendo lolote lile lililoainishwa katika kifungu cha 26 cha sheria hii; kuzuia njia au barabara au mkondo wa maji; kufunika kisiki cha mti kwa majani au udongo au kwa njia yoyote ile, kuharibu au kuondoa kisiki hicho; na kuharibu, kuchafua, kubadilisha, kuweka wigo, alama ya mpaka au notisi au ubao wa matangazo katika mti. Sheria hii inamtaka mtuhumiwa wa kosa jukumu la kuthibitisha kutokutenda kosa.

  Hata hivyo sheria inasema wazi kuwa kitendo cha mtu kukutwa katika maeneo ya hifadhi ya msitu na kifaa chochote kile kinachoweza kutumika kukata, au kuchukua zao lolote la msitu ni kutenda kosa. Sheria inamruhusu Mkurugenzi wa Misitu kutoa tamko katika gazeti la serikali juu ya kutokuwa kosa kwa mtu yeyote yule anayekutwa na vifaa hivyo katika hifadhi nzima au sehemu yake.

  Ni lazima tamko hilo liwekwe katika sehemu iliyo wazi kwenye Ofisi za Halmashauri za Serikali za Mitaa/Vijiji ambako hifadhi husika ipo au iko karibu yake na litangazwe katika namna ambayo ni ya kawaida katika eneo hilo ili kuwawezesha wenyeji na wakazi wa eneo hilo kupata taarifa hiyo.

- Vilevile, kama mnyama yoyote wa kufugwa akikutwa anachungwa au anaingia katika hifadhi yoyote ile ya msitu, basi mnyama huyo atachukuliwa kuwa alichungwa katika hifadhi hiyo. Mwenye mnyama huyo atahesabiwa kuwa ndiye aliyeruhusu kuchungwa au kuingia kwake katika hifadhi hiyo kinyume cha sheria. Kukiuka masharti ya kifungu 84(1) (a)-(e) na 84(2)-(3) ni kosa la jinai na mtu huyo pindi akikutwa na hatia atatozwa faini kati ya shilingi elfu thelathini na shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi miaka miwili au kupewa adhabu ya kifungo na faini.

- Kwa mujibu wa kifungu cha 85 ni kosa la jinai kwa mtu yeyote asiye na leseni au kibali kutoka mamlaka husika, kuangusha, kukata, kuharibu, kuondoa au kuuza mti uliotunzwa au kuhifadhiwa au sehemu yake kutoka katika ardhi isiyohifadhiwa. Adhabu ya kosa hili ni faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi mwaka mmoja. Mwenye hatia anaweza kupewa adhabu zote mbili yaani faini na kifungo.

- • Kifungu cha 86 cha sheria hii kinatamka kuwa ni kosa la jinai kwa mtu yeyote yule, bila ruhusa au kibali kutoka kwa mamlaka husika, na kwa mujibu wa sheria hii; kuchuma, kuondoa, na kuchukua sampuli au kwa namna yoyote ile na kwa makusudi kutoa sumu, kuharibu au kuteketeza mimea-pori iliyoorodheshwa; kuonyesha kwa ajili ya kuuza au kununua au kuwa au kumiliki mimea pori iliyoorodheshwa; kuuza nje ya nchi au kujaribu kuuza nje ya nchi mimea pori au sehemu yake au mbegu zake;

Adhabu ya kosa hili ni faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi sita na kutozidi miaka miwili. Mwenye hatia anaweza kupata adhabu zote mbili za faini na kifungo. Kifungu cha 87 kinataka makosa yote yanayohusiana na wanyamapori yashughulikiwe kwa mujibu wa sheria zinazohusika na mambo ya wanyamapori na sheria nyinginezo.

- Kwa mujibu wa kifungu cha 88 ni kosa la jinai kwa mtu yeyote yule, asiye na ruhusa au baraka za mamlaka husika, kukutwa na mazao ya misitu, isipokuwa kama ataweza kuthibitisha kuyapata kwake kihalali au kwa namna isiyo na kosa. Jukumu la kuthibitisha kutokuwa na hatia liko kwake. Adhabu ya kosa hili ni faini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja. Kwa mujibu wa kifungu cha 89 ni kosa la jinai kwa mtu yeyote, asiye na ruhusa halali au sababu:

- Kuvuna mazao ya misitu kwa mujibu wa sheria hii;
- Kuendesha au kusababisha kuendeshwa kwa gari na kuchukua, kubeba, kuondosha, au kusafirisha mazao ya misitu kinyume na sheria hii;
- Kuchukua, kubeba au kuondosha kwa njia isiyo kwa chombo cha moto mazao yoyote ya misitu kinyume na sheria hii;
- Kutaka kuuza, kuuza au kununua mazao ya misitu kinyume cha sheria hii;
- Kuhifadhi mazao ya misitu kinyume cha sheria hii;
- Kuweka alama za ubora na viwango katika mbao yoyote ile wakati si mtu mwenye dhamana hiyo; na
- Kuuza nje ya nchi au kuiingiza zao la misitu katika mauzo ya nje, ambalo uuzaji wake nje ya nchi unahitaji cheti husika cha uuzaji nje, bila ya kuwa na cheti sahihi cha uuzaji nje.

Dhamana au jukumu la kuthibitisha kutokuwa na hatia kwa mtuhumiwa liko kwa mtuhumiwa. Adhabu ya kosa au makosa haya ni faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja ama kifungo kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili. Kifungu cha 90 kinatamka kuwa ni kosa la jinai kwa mtu yeyote yule kufanya mambo yafuatayo:

- Kughushi, kubadilisha, kuharibu au kufuta au kuharibu stempu, alama, leseni, kibali, cheti, ruhusa, au risiti iliyotumika au kutolewa kwa mujibu wa sheria hii au kanuni, amri, au taarifa iliyotolewa au kutungwa kwa mujibu wa sheria hii;

- Kwa udanganyifu na bila ruhusa au mamlaka halali kutumia au kutoa stempu, alama, leseni, kibali, cheti, ruhusa, au risiti iliyotumika au inayokusudiwa kutumika au kutolewa kwa mujibu wa sheria hii au kanuni, amri, au taarifa iliyotolewa au kutungwa kwa mujibu wa sheria hii;

- Kuweka alama kwenye mbao, iwe mbao hiyo imewekwa alama na mweka alama aliyeruhusiwa au mkaguzi au hapana, au kuweka alama sawa na ile inayotakiwa na sheria hii au sheria ndogo iliyotungwa kwa mujibu wa sheria hii na kuweza

kuifanya kuchukuliwa kuwa ni alama inayotakiwa na sheria hii.

Pindi akikutwa na hatia mtuhumiwa atapigwa faini isiyopungua shilingi milioni moja na kutozidi shilingi milioni tatu au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili. Mahakama inaweza kumpa adhabu zote mbili yaani faini na kifungo.

Kifungu cha 91 kinaweka wazi kuwa mtu yeyote ambaye bila ruhusa halali ya kisheria:

- Anawasha, au kusaidia kuwasha au kutumia au kuchochea au kuongeza mafuta katika moto au kusababisha mambo haya kutokea;
- Anaacha bila uangalizi moto ambao bila ruhusa au kwa ruhusa amewasha au amesaidia kuuwasha au kutumia, kuchochea, au kuongeza mafuta bila kuhakikisha kuwa moto huo umezimwa kabisa;
- Ameshindwa kufuata au kutekeleza amri halali iliyotolewa kwake kuhusiana na Sehemu ya Tisa ya sheria hii: ana hatia ya kosa na pindi atakapotiwa hatiani atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingielfu hamsini na kutozidi shilingi milioni moja au adhabu ya kifungo kisichozidi mwakammoja ama kupewa adhabu zote mbili.

Kifungu cha 91(2) kinatamka wazi kuwa mtu yeyote yule ambaye kwa makusudi na kwa kinyume cha sheria anawasha moto katika hifadhi ya msitu, shamba la misitu, miti iliyomea, mche, vichaka, viwe au visiwe ni vya asili anatenda kosa la jinai na pindi akikutwa na hatia atapewa adhabu kama ilivyoanishwa na kifungu cha 321 cha Sheria ya Makosa ya Jinai.

- Pia ni kosa kutenda kosa hilo katika misitu iliyo katika ardhi ya kijiji ambayo inamilikiwa na mtu mmoja au watu wengi kwa mujibu wa hati miliki ya ardhi ya kimila; na Misitu katika ardhi ya jumla au ya kijiji ambayo umiliki wake ni kwa mujibu wa hati iliyotolewa kwa mtu au kampuni au ushirika kwa ajili ya kuitunza kwa mujibu wa sheria hii.

3.3 Makosa na adhabu katika sheria za wanyamapori

Mtu yeyote akifanya mambo yafuatayo atakuwa amevunja Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori na atapaswa kupata adhabu kulingana na kosa alilofanya. Makosa hayo ni kama yanavyoainishwa hapa chini:

- Si ruhusa mtu kuwinda wanyamapori bila kuwa na leseni inayomruhusu kufanya hivyo.
- Endapo mtu ana leseni, si ruhusa kuwinda mnyama ambaye hajaruhusiwa kulingana na leseni, wala kuwinda zaidi ya idadi inayotajwa katika leseni ya uwindaji.

  Na endapo mtu atakuwa na hatia ya makosa hayo atahukumiwa kifungo cha miaka 3-5 kulingana na aina au kulipa fidia au vyote kifungo na fidia.
- Mtu yoyote hana ruhusa ya kumjeruhi mnyama yeyote na endapo atamjeruhi katika harakati za uwindaji, mwindaji anapaswa kuhakikisha anamuua mnyama aliyemjeruhi kwa muda mfupi uwezekanao.
- Mtu yeyote atakayemjeruhi mnyamapori, atapaswa kulipa fidia ambayo ni sawa na mara mbili ya bei ya mnyama aliyejeruhiwa au kufungwa jela kwa muda usiopungua miezi 12.
- Mtu yeyote asiye na leseni hapaswi kumiliki wala kuuza nyara za serikali, na mtu yoyote atakayekutwa anamiliki nyara za serikali kinyume na sheria na kukutwa na hatia anaweza kuhukumiwa kifungo kisichopungua miaka 20 na kisichozidi miaka 30 au kulipa fidia yenye thamani mara mbili mpaka mara kumi zaidi ya thamani ya nyara alizokutwanazo, au fidia pamoja na kifungo.
- Vilevile mtu yeyote anayefahamu mtu anayemiliki nyara za serikali kinyume na sheria, ana wajibu wa kutoa taarifa kwenye mamlaka ya hifadhi, asipofanya hivyo, atakuwa amevunja sheria na atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilling laki tano au kifungo kisichopungua miezi 12 na kisichozidi miezi 18 au vyote, yaani kifungo pamoja na malipo, na

- Mwindaji mwenye kibali cha kuwinda, hana ruhusa ya kuwinda wanyama wadogo au wakike na wenye mimba, kufanya hivyo ni kosa kisheria. Vilevile hana ruhusa kuwinda kwa kutumia mbinu za uwindaji zilizokatazwa. Akifanya hivyo, pamoja na adhabu nyinginezo, mamlaka inaweza kumfutia leseni.

  Ni vyema wananchi wafahamu kuwa, kukutwa na silaha pekee katika maeneo ya hifadhi ni kosa kisheria, na mahakama itamhukumu mtu huyo kama mtu ambaye anataka kuwinda hata kama hajakutwa na kitu kingine kinachoonesha kama kweli alikuwa anawinda au la.

USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA USIMAMIZI WA MISITU NA WANYAMAPORI

SURA YA KWANZA
USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA USIMAMIZI WA MISITU NA WANYAMAPORI

1.0. Utangulizi

Usimamizi wa maliasili, hususani misitu na wanyamapori, kwa muda mrefu umekuwa chini ya Serikali Kuu kama mwamuzi mkuu wa nini kitekelezwe na ngazi mbalimbali za kiutendaji zilizoko chini yake kama vile Halmashauri za Wilaya na Vijiji. Usimamizi wa aina hii umejikita katika kuhakikisha kuwa malengo ya uhifadhi ndiyo yanapewa kipaumbele.

Pamoja na mchango mkubwa wa wananchi, hasa waishio karibu na maliasili kama vile misitu na wanyamapori, tatizo kubwa limekuwa ni faida ndogo wanayoipata kutokana na rasilimali hizo. Wanajiona kuwa maliasili hizo si zao na hazina manufaa kwao.

Sura hii inaainisha dhana ya ushiriki wa wananchi katika usimamizi wa rasilimali na namna ambavyo ushiriki wao ni muhimu na unapaswa kutekelezwa kwa vitendo na taasisi za kiutendaji.

1.1 Misingi ya Utawala bora katika Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori

Utawala bora ni jambo la msingi katika kuleta usimamiziwa maliasili wenye tija. Misingi ya Utawala bora ni pamoja na:

- Uwajibikaji;
- Uwazi;
- Ushirikishwaji; na
- Utawala wa sheria.

Misingi iliyotajwa hapo juu inalenga kuhakikisha kuwa maamuzi na maazimio yote yanayoathiri maliasili za misitu na wanyamapori na watumiaji wa maliasili hizo yanatekelezwa kikamilifu ili kuhakikisha kuwa kuna utendaji wenye tija na unaozingatia haki za msingi za binadamu.

1.2 Ushiriki ni nini?

Ushiriki ni mchakato wa mtu au kundi la watu kuhusika katika kutoa au kuchangia maoni na kuwa sehemu ya maamuzi katika masuala mbalimbali ya umma, kwa mfano mambo yanayohusu siasa, uchumi, usimamizi, pamoja na maamuzi mengine ya kijamii.

Aidha ushiriki ni kitendo cha kutoa fursa kwa makundi yanayoathiri au yanayoathiriwa na maliasili (misitu na wanyamapori), katika ulinzi, usimamizi, uhifadhi na utekelezaji wa miradi mbalimbali inayozunguka maliasili husika.

Ibara ya 21(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania inatoa haki kwa kila mtu kushiriki kwa ukamilifu katika mambo yote yanayomhusu yeye, jamii na taifa. Hivyo

basi ushiriki ni haki ya kikatiba. Aidha, Katiba inamtaka kila raia kushiriki kikamilifu katika kulinda mali ya Jamhuri ya Muungano kama vile misitu na wanyamapori.

Dhana ya ushiriki wa wananchi katika kulinda na kusimamia maliasili imefafanuliwa vizuri na ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Ibara hii ndiyo inayomtaka kila raia kushiriki katika kulinda maliasili za nchi na mali ya umma na kupiga vita ubadhirifu na matumizi mabaya ya rasilimali za Taifa.

Kwa msingi huu, wananchi wa Tanzania wana haki ya kikatiba kushiriki katika miradi mbalimbali ya kimaendeleo na ya usimamizi wa rasilimali zao kama vile misitu na wanyamapori.

1.2 Umuhimu wa Kushiriki katika Usimamizi wa misitu na wanyamapori

Ushiriki wa wananchi unawawezesha kufanya yafuatayo:

- Kushiriki katika kulinda, kutunza na kusimamia misitu na wanyamapori na hivyo kuwa sehemu ya maendeleo ya rasilimali hizo;
- Kupanga, kusimamia, na kutekeleza miradi ya maendeleo katika maeneo yao;
- Kuhoji utendaji wa serikali katika ngazi mbalimbali;
- Kuhoji juu ya mapato na matumizi ya fedha zinazotokana na rasilimali za misitu na wanyamapori;
- Kunufaika na matumizi na huduma za kimazingira za maliasili hizo;
- Kuhakikisha kuwa makundi yote ndani ya jamii kama vile wanawake, walemavu na wazee wanapata fursa sawa katika kusimamia rasilimali; na
- Kushirirki kikamilifu katika kutoa maoni juu ya sera, sheria na kanuni mbalimbali zihusuzo usimamizi wa rasilimali hizo.

1.2.1 Ushiriki wa Wananchi Katika Usimamizi Wa Misitu

Rasilimali za Misitu zinahitaji usimamizi endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Kwa muda mrefu misitu ya Tanzania ilisimamiwa bila ushiriki kamili wa wananchi na wadau wengine wanaozunguka misitu.

Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu (PFM) wa mwaka 2001 unazipa jamii mamlaka ya kupanga, kutekeleza na kusimamia mistu. Ni mpango unaolenga kuyaweka maeneo mengi ya misitu chini ya usimamiziwa wananchi ili kupanua wigo wa wananchi kunufaika na kuwa sehemu ya mipango na maamuzi yahusuyo misitu. Mpango huu huhusisha misitu inayohifadhiwa na kijiji ndani ya ardhi ya kijijij (CBFM) na ile inayohifadhiwa na mwekezaji au Serikali (PFM) kwa lengo la uvunaji au utunzaji wa uhainuwai. Mpango huu unaweka wazi majukumu ya wadau wote.

Mpango waUsimamizi Shirikishi wa Misitu umeanzishwa kisheria, na umerasimishwa na vyombo vifuatavyo;

- Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998,
- Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu wa Mwaka 2001
- Sheria ya Misitu namba 14 ya Mwaka 2002, na
- Kanuni ya Uendeshaji wa Misitu ya Mwaka 2004.

1.3.2 D hana ya Ugatuaji wa Madaraka katika Utekelezaji wa Miradi Shirikishi

Ugatuaji wa madaraka ni jitihada za Serikali zinazolenga kuongeza ushiriki wa wananchi katika kutekeleza na kusimamiarasilimali za misitu na wanyamapori.

Katika juhudi za kutekeleza dhana ya ugatuaji, mipango, bajeti na programu hujumuishwa na mipango na bajeti za maendeleo za sekretarieti za mikoa na serikali za mitaa. Mipango ya utekelezaji huibuliwa na wananchi kwa kutumia mbinu ya fursa na vikwazo kwa maendeleo (O & OD).

1.3.3 Haki na Wajibu wa Wadau Mbalimbali

Mpango Shirikishi wa Usimamizi wa Misitu unatoa haki na wajibu kwa wadau wote wanaohusika kama vile Halmashauri za Wilaya, Vijiji na wananchi. Misitu sasa inamilikiwa kwa pamoja kupitia Halmashauri za Vijiji pamoja na mamlaka za wilaya.

Mpango huo unatoa haki na wajibu kwa vijiji kama ifuatavyo:

- Wanakijiji wanaweza kuvuna rasilimali za misitu ili mradi matumizi ya Misitu yawe endelevu;
- Kamati ya Maliasili inalazimika kufuatilia hali ya misitu pamoja na matumizi yake ili kuhakikisha kuwa matumizi hayazidi viwango vifaavyo; na
- Serikali ya kijiji na Kamati ya Maliasili wanaweza kutumia sheria ndogo ndogo pamoja na vibali, ada na faini ili kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu.

1.4 Ushiriki wa Wananchi Katika Usimamizi wa Wanyamapori.

Sekta ya wanyamapori ni chanzo kikubwa cha fedha za kigeni na ajira nchini lakini bado maendeleo yake ni duni ikilinganishwa na umuhimu wake. Mfumo wa sasa wa matumizi ya wanyamapori umejikita zaidi katika utalii, uwindaji, na ukamataji wa wanyamapori. Hata hivyo mfumo huu haujachagiza kukua kwa sekta nyingine kiuchumi kama vile kilimo, ranchi na miradi ya matumizi ya ardhi vijijini kutokana na kutofungaminishwa nazo.

Sera na sheria zinazohusu wanyamapori nchini zinatoa fursa kwa wananchi kushiriki katika usimamizi wa wanyamapori. Sheria ya Wanyampori ya Mwaka 2009 inaruhusu vijiji kuanzisha Jumuiya za Usimamizi wa Wanyampori (WMA) katika ardhi za vijiji. Hii inalenga kutoa fursa kwa wananchi kunufaika moja kwa moja na rasilimali hizi. Sheria inatoa fursa hii ili kuwezesha vijiji kuendelea kupata faida za kiuchumi kutokana na wanyamapori ikiwa ni njia ya kuleta maendeleo vijijini. Pia, sheria inaruhusu kuanzishwa kwa Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu ambayo yamekuwa chini ya usimamizi wa Serikali kwa kuwashirikisha wananchi. Aidha, mamlaka mbalimbali zenye dhamana ya kuhifadhi wanyamapori kupitia programu mbalimbali zimekuwa zikiwashirikisha wananchi katika uhifadhi na usimamizi wa wanyamapori mfano Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA).

Pia, Sera ya Wanyamapori inahimiza kuunganishwa hifadhi ya wanyamapori na maendeleo ya vijijini kwa:

- Kukuza matumizi halali ya wanyamapori na mazao yake; na
- Kuhimiza biashara halali na endelevu ya wanyamapori na mazao yake kutoka kwenye Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa na hivyo kuwapatia wanyamapori thamani kubwa ya kibiashara huku yakizingatiwa matumizi endelevu ya aina za wanyama wauzwao.

  Ingawa Serikali ina mikakati shirikishi inayoendelea kama vile Uhifadhi wa Kijamii (CBC), (Idara ya Wanyamapori), Ujirani Mwema (TANAPA), na Maendeleo ya Jamii (Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro), namna na kiwango cha ushiriki wa wananchi bado havijakidhi mahitaji na kuwafanya wananchi na jamii husika kama wadau wa kweli wa rasilimali hizi.

Pic 1

Wadau wa miradi Shirikishi ya Wanyamapori Tanzania

- Serikali Kuu;
- Halmashauri za Wilaya;
- Serikali za Vijiiji na kamati zao za maliasili; na
- Wananchi.

CHANGAMOTO KATIKA USIMAMIZI WA MISITU NA WANYAMAPORI

2.0. Utangulizi

Sura hii inaainisha changamoto na migogoro inayokabili sekta ya misitu na wanyamapori. Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kuondoa migogoro kwenye sekta bado zipo changamoto mbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa zinadhoofisha jitihada hizo.

Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili: sehemu ya kwanza inaainisha changamoto zilizopo katika usimamiziwa maliasili nchini ikiwa ni pamoja na migogoro inayojitokeza katika mchakato mzima wa usimamizi wa misitu na wanyamapori. Sehemu ya pili inatoa ufafanuzi juu ya maana na aina ya migogoro iliyopo katika usimamizi wa maliasili ikiwa ni pamoja na mapendekezo juu ya nini kifanyike ili kukabiliana na changamoto hizo.

2.1. Changamoto katika Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori

Baadhi ya changamoto zinazoikumba sekta hii ni pamoja na:

2.1.1. Kukinzana kwa Sheria

Sheria mbalimbali za usimamizi wa misitu na wanyamapori kukinzana na hivyo kukwamisha utekelezaji wake. Sehemu hii inaainisha kwa ufupi namna sheria zinavyokinzana.

Sheria ya Ardhi ya Kijiji Namba 5 ya Mwaka 1999 inatoa mamlaka kwa Halmashauri za Vijiji kuwa vyombo vikuu vya usimamizi wa ardhi za vijiji. Hata hivyo Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002 kupitia kanuni zake inampa mamlaka Afisa wa Misitu wa Wilaya kutoa vibali vya uvunaji wa misitu hata ile iliyopo kwenye ardhi ya kijiji. Kitendo hiki kinaondoa mamlaka kwa Halmashauri za Vijiji kusimamia ardhi ya kijiji na rasilimali za misitu. Aidha utaratibu mzima wa kuanzishwa kwa hifadhi za misitu za vijiji chini ya Sheria ya Misitu ya Mwaka 2002 unapingana na utaratibu na mamlaka ya serikali za vijiji kama ulivyoanishwa na Sheria ya Ardhi ya Kijiji ya Mwaka 1999 na Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 2007. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Kijiji serikali ya kijiji inaweza kutenga eneo la pamoja na kulifanya kuwa hifadhi kwa kibali cha Mkutano Mkuu. Hii ni tofauti na matakwa na Sheria ya Misitu inayotaka uanzishaji wa Hifadhi za Misitu ya Kijiji kupata kibali cha Mkurugenzi wa Misitu.

Vile vile, uanzishwaji wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) katika ardhi za vijiji chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 2009 na kanuni zake za mwaka 2012 ni changamoto kisheria kwani Jumuiya Zilizoidhinishwa (AAs) zinatakiwa kuwajibika kwa Halmashauri za Vijiji lakini kiutendaji Jumuiya hizo bado ziko juu ya Halmashauri za Vijiji kwa sababu jumuiya zilizoidhinishwa huwajibika kwa Afisa Wanyamapori wa Wilaya kutokana na ukweli kwamba Jumuiya hizo zinaundwa na Vijiji zaidi ya kimoja. Hii inaondoa mamlaka ya Halmashauri za Vijiji katika kusimamia ardhi ya vijiji na hivyo kusababisha migogoro isiyoisha.

2.1.2. Mgongano wa Mamlaka za Kiutendaji katika Taasisi za Serikali

Pamoja na sheria kuanzisha taasisi mbalimbali za uhifadhi na usimazmizi wa misitu na wanyamapori nchini kama vile Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) na watendaji mbalimbali kwenye Halmashauri za Wilaya na Vijiji, taasisi hizi zimekuwa zikitoa maamuzi yanayokinzana na hivyo kudhoofisha jitihada za usimamizi wa maliasili.

Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 2009 inaelekeza kuwa mtalii au mwindaji wa ndani anaruhusiwa kuwinda ndani ya Pori la Akiba, Pori Tengefu, na Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori, hata hivyo inapotokea mwindaji amemjeruhi mnyama katika harakati za uwindaji, mwindaji anapaswa kuhakikisha anamuua mnyama huyo katika muda mfupi iwezekanavyo lakini pale ambapo mnyama amepigwa na kujeruhiwa na kupata mwanya wa kuingia katika Hifadhi ya Taifa, basi hairuhusiwi tena kuwindwa kwani Sheria ya Hifadhi za Taifa hairuhusu uwindaji ndani ya Hifadhi hizo.

Chanzo cha migogoro kiutendaji ni pamoja na mapungufu yaliyopo kwenye sheria za sasa, watendaji kuingilia majukumu ya watendaji wengine kwa makusudi na kukosekana kwa azma ya kujenga mfumo ulio wazi na huru hususani kuhusu mamlaka mbalimbali za kiutendaji kwenye taasisi za Serikali.

Migogoro mingine ni kutokutambulika, kuheshimika na kudharauliwa kwa mamlaka ya kisheria ya serikali za vijiji juu ya ardhi na rasilimali mbalimbali ikiwemo misitu na yafanyakwo na taasisi za serikali kuu, halmashauri za wilaya na kampuni binafsi. Maamuzi mengi ya matumizi ya rasilimali za misitu, wanyamapori, na madini katika ardhi za vijiji yamekuwa yanafanywa na idara za serikali kuu bila kutambua kuwa serikali za vijiji zinapaswa kushirikishwa kikamilifu kuyafikia. Kwa mfano uanzishwaji wa vitalu vya uwindaji katika ardhi za vijiji ufanywao na Idara ya Wanyamapori ni batili kwa kutokushirikisha serikali za vijiji.

2.1.3. Ushiriki mdogo wa Wananchi katika Kutoa Mawazo yao na Kusimamia Kikamilifu Utunzaji na Uhifadhi wa Misitu na Wanyamapori

Pamoja na ukweli kuwa wananchi ndio walio karibu sana na rasilimali hizi na kwamba sheria zinatoa fursa kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha kuwa rasilimali za nchi zinasimamiwa vizuri, bado wananchi hawapewi fursa ya kushiriki katika maamuzi mengi yanayohusu uhifadhi na usimamizi wa rasilimali hizo.

Maamuzi mengi yanayohusu uhifadhi na usimamizi wa misitu na wanyamapori yanatolewa na viongozi na kupelekwa kwa wananchi kwa ajili ya utekelezaji. Vile vile, wananchi wanaoishi karibu na maliasili kama hifadhi za wanyamapori na misitu hawapewi nafasi za kutosha kushiriki katika uandaaji wa mipango, miongozo, sera, na kanuni ambazo utekelezaji wake

unawaathiri kwa namna moja ama nyingine. Kutokana na ushiriki mdogo kumekuwa na migogoro ya mara kwa mara kati ya Serikali na wananchi kwa upande mmoja na kati ya wananchi na wawekezaji kwa upande mwingine.

2.1.4. Ukiukwaji wa Sheria za Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori.

Moja ya changamoto zinazokabili usimamizi wa maliasili nchini ni kukithiri kwa vitendo vya ukiukwaji wa sheria. Pamoja na kuwepo kwa Sheria mbalimbali za uhifadhi na usimamizi wa maliasili kwa mfano, Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 2009 inayozuia vitendo vya kuua na kutorosha wanyama bila ridhaa ya mamlaka husika, sheria hizi zimekuwa zikikiukwa kwa makusudi na baadhi ya watendaji wa Serikali. Mfano mzuri ni kitendo cha utoroshwaji wa Twiga kutoka Hifadhi ya Serengeti kupitia Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA) kwenda katika nchi za Uarabuni.

Kukithiri kwa biashara ya pembe za ndovu kutoka Tanzania kwenda nchi za nje ni moja ya sababu za kuuawa kwa tembo wengi katika Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na kwenye Mapori Tengefu. Ongezeko la biashara hii ni kiashiria kingine cha ukiukwaji wa sheria unaofanywa na watendaji wa Serikali waliopewa dhamana ya kusimamia wanyama hawa kwa manufaa ya nchi yetu. Vilevile, misitu inakabiliwa na ongezeko la uvunaji haramu wa mbao na uchomaji ovyo wa mkaa kinyume cha sheria huku nchi yetu ikikoseshwa kiwango kikubwa sana cha mapato.

2.1.5. Ukosefu waRasilimali za Kutosha katika Kusimamia na Kuhifadhi Misitu na Wanyamapori.

Pamoja na mchango mkubwa wa sekta hii katika pato la taifa, bado sekta hii inakabiliwa na changomoto ya ukosefu wa rasilimali watu na rasilimali fedha katika kukidhi mahitaji yake. Baadhi ya watendaji katika sekta

ya wanyamapori na misitu hawana vitendea kazi vya kutosha na hivyo kukwamisha doria kwenye maeneo ya hifadhi jambo ambalo limechangia kuongezeka kwa vitendo vya ujangili, uvunaji haramu wa mbao, uchomaji ovyo wa mkaa na shughuli nyingine zinazofanyika kinyume cha sheria. Aidha, baadhi ya watendaji wa sekta hii hawana elimu na ujuzi wa kutosha kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

2.1.6. Kutokuwepo kwa Mgawanyo Sawa wa Mapato kati ya Serikali na Wananchi

Kama ilivyoainishwa katika sura zilizotangulia, uhifadhi na utunzaji wa misitu na wanyamapori ni jukumu la kila mwananchi, hivyo ni wajibu kwa kila mwananchi kuhakikisha anashiriki kikamilifu katik kusimamia rasilimali hizi. Wananchi wamekuwa wakishiriki katika uhifadhi na utunzaji wa misitu na wanyamapori kupitia njia mbali mbali, hata hivyo wananchi hawanufaiki na mapato yatokanayo na ushiriki wao.

Kutonufaika na rasilimali hizi ipasavyo kunawavunja moyo wananchi na jamii zinazizozunguka na hivyo kusababisha kutokushiriki kwao katika jitihada za kuzuia uvunaji haramu wa mazao ya misitu na wanyamapori nchini. Changamoto hii pia imesababisha kuendelea kukithiri kwa migogoro katika matumizi ya ardhi hususani kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi za wanyamapori na misitu.

2.2. Maana na Aina za Migogoro katika Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori.

Migogoro inaweza kufafanuliwa kuwa ni hali ya kutoelewana/kutoafikiana baina ya pande mbili juu ya jambo fulani. Katika sekta ya maliasili, migogoro hii kwa kiasi kikubwa inachangiwa na kutofautiana kimtazamo, kifikra, na hata kiutendaji kati ya mtu mmoja na mwingine, kundi moja la watu na kundi jingine juu ya uhifadhi na usimamizi wa misitu na wanyamapori.

Zifuatazo ni baadhi ya aina mbalimbali za migogoro katika usimamizi wa misitu na wanyamapori:

2.2.1. Migogoro kati ya Wananchi na Mamlaka za Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori.

Kumekuwa na migogoro mingi kati ya wananchi na mamlaka za usimamizi wa wanyamapori nchini. Baadhi ya sababu za kuongezeka kwa migogoro ni kutokana na ukiukwaji wa makusudi wa sheria na watendaji wa Serikali; wananchi kuingia kwenye maeneo ya hifadhi za misitu na wanyamapori kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kimaendeleo kinyume cha sheria; na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu mchango wa misitu kwa maendeleo ya nchi kwa ujumla

2.2.2. Migogoro Inayosababishwa na Baadhi ya Rasilimali za Maliasili kama Wanyama Kuvamia Mashamba ya Wananchi na Kuharibu Mazao.

Kwa kipindi kirefu kumekuwa na migogoro katika usimamizi wa misitu na

wanyamapori unaosababishwa na wanyamapori kuharibu mazao ya wananchi. Migogoro hii imesababisha wanyama wengi kuuawa kama vile tembo, viboko na nyati.

Migogoro mikubwa hutokea pale ambapo mamlaka husika zinachelewa na wakati mwingine kushindwa kushughulikia madai ya fidia kwa wananchi kutokana na uharibifu huo. Wakati mwingine fidia inayotolewa kutokana na uharibifu wa mazao, vifo na hata kujeruhiwa kwa wananchi ni ndogo ikilinganishwa na ukubwa wa madhara.

2.2.3. Migogoro ya Wananchi na Serikali kuhusu Mapato Yatokanayo na Misitu na Wanyamapori.

Pamoja na sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali kuweka taratibu za wananchi kunufaika kutokana na ushiriki katika usimamizi wa maliasili, bado suala la mapato kidogo kwa wananchi limeendelea kuikabili sekta hii. Kwa mfano, katika Programu za Usimamizi Shirikishi wa Misitu (PFM) kiasi cha mapato kinachopatikana ni kidogo ukilinganisha na mchango mkubwa unaotolewa na wananchi katika usimamizi wa rasilimali hizi. Aidha, baadhi ya wananchi wanaamini kuwa miradi ya maji inayotokana na jitihada za wananchi kusimamia vizuri misitu inapelekwa maeneo ya mijini na kuwaacha wananchi wa vijijini wakihangaika kupata maji wakati wao ndio wanaotunza na kuhifadhi misitu ambayo ni chanzo cha maji. Hali hii pia inaleta migogoro na kudhoofisha dhana ya usimamizi shirikishi wa maliasili hizi.

2.3. Athari za Migogoro katika Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori

Kuna athari nyingi ambazo zinatokana na kukithiri kwa migogoro katika usimamizi wa maliasili nchini. Baadhi ya athari hizo zimeainishwa hapa chini:

2.3.1. Kudhoofika kwa Mchakato au Jitihada za Usimamizi wa Misitu na Wanyamapori;

Kuwepo kwa migogoro mingi katika usimamizi wa maliasili ni chanzo kikubwa cha kurudisha nyuma jitihada za kusimamia na kuhifadhi maliasili nchini. Hii inatokana na ukweli kwamba wananchi wengi ambao ni wadau wakubwa katika usimamizi wa maliasili wamekuwa wakikosa ari ya kuendelea kushiriki katika michakato hiyo na hivyo kusababisha kuongezeka kwa ujangili na biashara haramu ya mazao ya misitu.

2.3.2. Kuharibika kwa rasilimali za Misitu na Wanyamapori ikiwa ni pamoja na kuharibiwa kwa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyapori.

Kutokana na migogoro mingi rasilimali za wanyamapori na misitu ikiwa ni pamoja na vyanzo vya maji imekuwa vikiharibiwa sana na kusababisha gharama kubwa za kusimamia na kuhifadhi maeneo yaliyoharibiwa. Uharibifu huu mbali na kusababisha gharama kubwa kwa Serikali kukabiliana nao pia umeendelea kukwamisha juhudi za uhifadhi katika maeneo mengi nchini. Kushuka kwa shughuli za utalii nchini kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na uharibifu wa Hifadhi za Taifa na maeneo mengine muhimu yenye vivutio vingi kwa watalii.

2.3.3. Kutokea kwa Vifo na Kujeruhiwa kwa Baadhi ya Wananchi.

Serikali imekuwa ikijitahidi kutatua migogoro hii japo ni ukweli usiopingika kwamba pamoja na jitihada hizi za Serikali yapo maeneo mengi nchini ambayo wananchi wamepoteza uhai na wengine kujeruhiwa vibaya. Mfano mzuri ni Loliondo, Kilombero, Kilosa, na Lindi. Chanzo kikubwa cha migogoro hii ni ardhi na kutokuwepo kwa utaratibu mzuri wa uainishaji wa matumizi mbalimbali ya ardhi hususani shughuli za kilimo na ufugaji.

Misitu na wanyamapori ni mali ya wananchi. Ushiriki wa wananchi ni haki ya msingi ya kisheria na kikatiba ili kujenga mfumo wa uwazi na uwajibikaji ambayo ni misingi ya usimamizi bora wenye tija. Ni jukumu la kila mwananchi kushiriki kikamilifu katika kusaidia kukua kwa sekta hii. Matumizi endelevu ya rasilimali hizi ni njia muhimu katika kuhakikisha kuwa wananchi kwa ujumla wananufaika nazo. Vyombo mbalimbali vyenye jukumu la usimamizi ni vyema vikatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria za nchi. Ushiriki mzuri katika usimamizi wa rasilimali ni ule unaotoa fursa kamilifu kwa wananchi katika kuamua juu ya matumizi ya rasilimali bila kuwepo kwa masharti yanayoondoa haki hii. Kuelewa majukumu ya wananchi na serikali na idara zake katika kuleta usimamizi bora wa rasilimali za wanyamapori, misitu na maliasili nyinginezo kutachagiza kukua kwa hivyo kuchangia kuleta maendeleo endelevu nchini.

USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI

"imetayarishwa na kuchapishwa na LEAT kwa ufadhili wa USAID kutoka kwa Watu wa Marekani".

Jengo la Mazingira, Mtaa wa Mazingira | Mikocheni B, S.L.P 12605 Dar es Salaam
Email: info@leattz.org | Simu 255-22-2780859 | Barua Pepe: info@leattz.org